**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**
**JESHI LA POLISI TANZANIA**

Anwani ya Simu: "MKUU POLISI"
Simu Namba: 026 2323585
Fax: 026 2323586
E – Mail: info.phq@tpf.go.tz

Ofisi ya Mkuu wa Jeshi la Polisi,
Makao Makuu ya Polisi,
4 Mtaa wa Posta,
S. L. P. 961,
**40483 DODOMA**

**18/06/2025**

## TAARIFA KWA UMMA
## KUHUSU KUPOTEA AU KUTOONEKANA KWA WATU MBALIMBALI NCHINI

Kumekuwepo na kuripotiwa kwa taarifa katika vituo vya Polisi na nyingine katika mitandao ya kijamii zikijulisha kwamba mtu au watu fulani wamepotea, hawaonekani au wamekamatwa na watu waliojitambulisha kuwa askari wa Jeshi la Polisi.

Jeshi la Polisi linapopokea taarifa hizo, huanza uchunguzi kwa kukusanya ushahidi kutoka vyanzo mbalimbali ili kupata ukweli wa taarifa ya nini kilichotokea kwani hauwezi kusema moja kwa moja kuwa mtu aliyeripotiwa kupotea, kutekwa, kulazimishwa kupotea au kuuawa bila ya kumpata anayedaiwa kupotea na ushahidi wa kuthibitisha taarifa hiyo ya nini kilichomtokea, kama alitendewa uhalifu ni nani wahusika, kulingana na sheria, kanuni na taratibu.

Vilevile, kwa mujibu wa kifungu cha 117 cha Sheria ya Ushahidi Sura ya 6 marejeo ya mwaka 2022 na kifungu cha 161 cha Sheria ya Ndoa Sura ya 29 marejeo ya mwaka 2019, dhana ya mtu kuchukuliwa kuwa amekufa inapaswa kuthibitishwa na mahakama baada ya miaka mitano kupita kulingana na vielelezo na ushahidi utakaowasilishwa.

Katika matukio ambayo yameripotiwa katika vituo vya Polisi na uchunguzi wa kina kufanyika na walioripotiwa kupotea kupatikana wakiwa hai na wengine wakiwa wamekufa, hadi sasa ushahidi kwa baadhi ya matukio yameonesha sababu zake ni kujiteka, wivu wa mapenzi, imani za kishirikina, kugombea mali, kulipiza kisasi, kwenda nchi nyingine kujifunza misimamo mikali na kukimbia mkono wa sheria baada ya kufanya uhalifu.

Miongoni mwa matukio hayo ambayo yamethibitishwa kwa sababu hizo ni pamoja na tukio la hivi karibuni lililomhusisha Shekhe Zuberi Said Nkokoo (53) mwalimu wa dini na kiongozi katika taasisi ya Islam Foundation iliyopo mkoani Singida ambayo pia inajishughulisha na

shughuli  za kuchinja wanyama. Katika tukio hilo kupitia vyombo mbalimbali vya habari ikiwemo mitandao ya kijamii kulisambaa taarifa za kutekwa kwa Shekhe huyo na watu aliowataja kuwa ni askari wa Jeshi la Polisi tarehe 02/06/2025 saa tano usiku akiwa na kiasi cha fedha taslimu shilingi za kitanzania milioni arobaini na mbili (Tshs. 42,000,000/=).Taarifa ya kupotea kwake pia iliripotiwa Polisi.

Baada ya uchunguzi, ilibainika kuwa  Shekhe Zuberi Said Nkokoo hakuwa ametekwa bali alitengeneza tukio la uongo la kutekwa ili kukimbia madeni aliyokuwa akidaiwa na watu mbalimbali (majina yao yamehifadhiwa) yenye jumla ya shilingi za kitanzania milioni mia tano ishirini na moja na laki tano (Tshs. 521,500,000/=). Shekhe Zuberi atafikishwa Mahakamani baada ya taratibu za kisheria kukamilika.

Baadhi ya matukio mengine yaliyohusishwa na utekaji wa watu vikihusishwa vyombo vya dola lakini baadae uchunguzi ukabaini kuwa vyombo vya dola havikuhusika kwenye matukio hayo ni pamoja na tukio la tarehe 07.06.2025 lililotokea katika Kijiji cha Mtakuja Kata ya Nanganga Wilaya ya Ruangwa Mkoa wa Lindi ambapo Ritha Severine Ndambalilo (41) Mkazi wa Dangote Mtwara, mfanyakazi wa kituo cha kuuza mafuta cha Kampuni ya Specialized Petrol Station ya Mtwara alikutwa akiwa ameuwa kwa kunyongwa na mtandio na kutupwa kando ya makarasha ya wachina katika Kitongoji cha Nahungo Kijiji cha Mtakuja Kata ya Malolo Wilaya ya Ruangwa. Upelelezi ulibaini kuwa mtu huyo aliuwawa na Juma Salum Nyenje (49) aliyekuwa akimtumia kama dereva wake wa bodaboda baada ya mtu huyo kumuona Ritha akiwa amebeba fedha kwenye mkoba wake. Kabla ya mwili wake kupatikana, taarifa zilisambaa kuwa alikuwa ametekwa na watu wasiojulikana. Watuhumiwa wawili (02) walikamatwa, kesi iko Mahakamani

Tukio lingine ni linamhusu Regina Rajabu Chaula (62) aliyekuwa na makazi Bahari Beach Kinondoni Dar es Salaam na nchini Dernmark aliyedaiwa kuuawa na Fred Rajabu Chaula na Bashiri Richard Chaula kisha mwili wake kutumbukizwa kwenye shimo la maji taka. Regina ambaye alikuwa na kesi za madai Mahakama Kuu Divisheni ya Ardhi dhidi ya watuhumiwa hao aliripotiwa kupotea ghafla Disemba 13, 2024 hadi tarehe 18.01.2025 mwili wake ulipokutwa kwenye shimo hilo la maji taka baada ya upelelezi wa Jeshi la Polisi. Watuhumiwa hao walikamatwa na kufikishwa mahakamani.

Pia, tarehe 11.11.2024 lilitokea tukio lililomhusu Bw. Deogratius Tarimo Mkazi wa Kibaha Mkoa wa Pwani ambaye alionekana kwenye picha mjongeo akipambana na watu waliotaka kumteka ambao hata hivyo walishindwa kutekeleza adhima yao hiyo. Taarifa

zilizosambazwa kwenye mitandao ya kijamii kuhusiana na tukio hilo zilisema kuwa waliokuwa wanatekeleza uhalifu huo ni askari Polisi. Uchunguzi ulibaini kuwa waliohusika sio askari Polisi na chanzo cha tukio hilo ni wivu wa mapenzi. Watuhumiwa sita (06) walikamatwa na kufikishwa Mahakamani.

Aidha, tarehe 24.08.2024 katika Kijiji cha Hyderere Kata ya Hyderere Tarafa ya Haydom Wilaya ya Mbulu, Mkoa wa Manyara, Saulo Samweli Balohho (44) Mkazi wa Hyderere alitoa taarifa ya uongo kwa kutumia simu ya mkononi kuwa ametekwa tangu tarehe 22.08.2024 na watu wasiojulikana na kumpeleka karatu mkoa wa Arusha kwa lengo la kumtoa Figo. Upelelezi ulibaini kuwa mtuhumiwa hakutekwa bali aliondoka nyumbani kwake akimuaga mke wake kwamba anapeleka fedha shilingi za kitanzania laki mbili na elfu themanini (Tsh.280,000/=) ukweni kwa mtoto wake wa kiume ambazo ni mahari aliyokuwa anadaiwa mtoto huyo. Uchunguzi ulibaini mtuhumiwa alizitumia fedha hizo na ili kuficha aibu akaamua kuzusha kwamba ametekwa. Mtuhumiwa alifikishwa mahakamani na kuhukumiwa kulipa faini ya shilingi za kitanzania laki moja (Tshs.100,000/=)

Tukio lingine ni la tarehe 23.08.2024 lililotokea katika Kitongoji cha Kwedijava Kijiji cha Nyasa Kata ya Kang'ata Tarafa ya Magamba Wilaya ya Handeni, Mkoa wa Tanga lililomhusisha Elia Elifaza Raymond Mchome (3) Mkazi Wa Kitongoji cha Kwedijava ambaye aliuawa na kufukiwa ndani ya chumba walichokuwa wakilala na Jackson Elisante Maeda (23) Mkazi wa Kwedijava kwa imani za kishirikina. Kabla ya kubainika kwa mwili wa mtoto huyo taarifa zilisambaa kuwa alikuwa ametekwa na watu wasiojulikana. Mtuhumiwa aliyehusika na mauaji haya alikamatwa na kesi iko Mahakamani.

Pia, tarehe 19.08.2024 Ezania Kamana (36) aliyetoweka bila kufahamika mahali alipokuwa, alikutwa akiwa ameuwawa na mpenzi wake aliyefahamika kwa jina la Abdallah Miraji Musa (42) kisha mwili wake kukatwakatwa na kuwekwa katika mifuko minne (04) ya Sandarusi na kutupwa maeneo ya Ununio. Mtuhumiwa alikamatwa, kesi iko mahakamani.

Kuna matukio ya watu saba ambao waliripotiwa Polisi Singida kuwa wamepotea/wametekwa. Tarehe 08.08.2024 Uchunguzi ulibaini katika Kijiji cha Ghalunyangu Kata ya Makuro Tarafa ya Mtinko Wilaya ya Singida, Mkoa wa Singida watu hao ambao ni Samwaja Sifael Said (22) na wenzake saba (07) waliuawa kwa kukatwa sehemu mbalimbali za miili yao kisha kunyofolewa au kutolewa baadhi ya viungo vya miili yao na kufukiwa kwenye mashimo tofauti tofauti na waganga wa kienyeji waliofahamika kwa majina ya Saidi Haji Msanghaa (24) Mkazi wa Kijiji cha Migungu pamoja na Kamba

Kasubi (34) wakishirikiana na wenzao 12. Aidha, baada ya ufuatiliaji ilibainika miili mingine mitatu (03) iliyofukiwa wilayani Chemba mkoani Dodoma na kufikisha jumla ya watu kumi (10) waliouawa na watu hao. Kabla ya kubainika miili yao taarifa zilisambaa kuwa watu hao walikuwa wametekwa na watu wasiojulikana. Watuhumiwa 13 walikamatwa, kesi iko Mahakamani.

Tarehe 31.07.2024 wafanyabiashara wawili wa Wilaya ya Songea, Mkoa wa Ruvuma waliofahamika kwa majina ya Ray James Hyera na Riziki Mbarara Mohamed walidaiwa kutekwa baada ya kutoonekana kwa siku kadhaa bila taarifa huku simu zao zikiwa hazipatikani. Upelelezi ulibaini kuwa watu hao waliuwawa na mganga wa kienyeji aliyefahamika kwa jina la Mtila Msua Ausi (29) Mkazi wa Ligunga Wilaya ya Tunduru, katika Pori la Mdingula Uwanja wa ndege kwa kuwanywesha sumu na yeye kuchukua pesa kiasi cha shilingi za kitanzania milioni kumi na tano (Tsh.15,000,000/=) ambazo marehemu walibeba na kwenda nazo kwa mganga huyo ili ziombewe dua. Watuhumiwa watatu (03) walikamatwa, kesi iko Mahakamani.

Tukio lingine ni la tarehe 03.07.2024, lililoripotiwa likiwahusu watoto wawili mmoja miaka (12) aliyekuwa Mwanafunzi wa darasa la saba katika Shule ya Msingi Busenga na mwingine miaka (08) aliyekuwa Mwanafunzi wa darasa la pili katika Shule ya Akiba English Medium iliyopo Wilaya ya Ilemela waliojiteka na kupanga nyumba katika eneo la Wilaya ya Nyamagana na kuanza kuwapigia simu wazazi wao kuwa wametekwa wako Buhemba mkoani Mara na watekaji wanahitaji shilingi za kitanzania laki moja (Tshs. 100,000/=). Watoto hao wanaendelea kufuatiliwa tabia zao chini ya Ustawi wa Jamii na Jeshi la Polisi.

Halikadhalika, tarehe 03.07.2024 John Zephania Mboge Mkazi wa Goba Center aliyekuwa akitokea Benki ya CRDB tawi la Coco Plaza alikamatwa na watu saba (07) na kumuingiza kwenye Gari lenye namba za usajili T.458 DYU Toyota kisha kumpora pesa. Watuhumiwa saba (07) walikamatwa na kufikishwa Mahakamani.

Tukio lingine ni la tarehe 17/06/2024 lililotokea katika Kitongoji cha Kabyonda Kijiji cha Mulele kata ya Ruhanga tarafa ya Kamachumu Wilaya ya Muleba Mkoa wa Kagera, ambapo mtoto aliyefahamika kwa jina la Noela Novat Asimwe (2.5) mwenye ulemavu wa ngozi aliripotiwa kutekwa na watu wasiojulikana. Uchunguzi wa Polisi ulibaini kuwa mtoto huyo ameuawa kwa kunyongwa shingo na kunyofolewa baadhi ya viungo vya mwili ikiwemo mikono yote miwili kisha mwili wake kutupwa kwenye daraja ukiwa umefungwa

kwenye mfuko wa sandarusi. Watuhumiwa tisa (09) akiwepo baba yake mzazi walikamatwa, kesi iko Mahakamani.

Katika tukio lingine la tarehe 15/05/2024 mtoto (Jina limehifadhiwa) aliripotiwa kutekwa katika maeneo ya Mwanjelwa Ilomba Wilaya ya Mbeya Mkoa wa Mbeya na Winfred Martin Komba (36) Mkazi wa Vingunguti Dar es Salaam kwa kushirikiana na mama mzazi wa mtoto huyo aitwaye Agnes Jacob Mwalubuli ikiwa ni njama waliyopanga ili kumshinikiza baba mzazi wa mtoto huyo atoe fedha za kitanzania milioni ishirini (Tshs. 20,000,000/=) ili mtoto aachiliwe na watekaji lasivyo watamuua. Watuhumiwa watatu (03) walifikishwa mahakamani na mtuhumiwa mmoja alihukumiwa kifungo cha miaka mitatu jela, mmoja alihukumiwa (mama mzazi) kifungo cha nje miezi 12 na Mama ambaye mtoto alikutwa kwake aliachiliwa huru.

Tarehe 12/02/2024 Buki Mdanzi Kizigina (52) Mkazi wa Magaoni Mkoa wa Tanga alidaiwa kutekwa na watu waliofahamika kwa majina ya Shilingi Saidi na Khalid Salim Mwarangi baada ya kudhulumiana kwenye biashara zao za dawa za kulevya na kwenda kumficha katika eneo la Putin wilayani Pangani, watuhumiwa walikamatwa na kufikishwa Mahakamani na Buki alipatikana akiwa hai.

Vilevile tarehe 06.11.2023 lililotokea tukio katika Kijiji cha Kemondo Wilaya ya Bukoba, Mkoa wa Kagera likimhusisha Amri Abdulahan (21) mkazi wa Kashai Manispaa ya Bukoba aliyejiteka mwenyewe kisha kutengeneza taarifa na kumdanganya baba yake mzazi kuwa ametekwa. Lengo likiwa ni kujipatia shilingi za kitanzania milioni tano (5,000,000/=). Uchunguzui wa Polisi ulibaini njama hizo na Mtuhumiwa alikamatwa na kufikishwa Mahakamani na alipatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo cha nje miezi 12

Tukio lingine ni la tarehe 15/7/2019 lililotokea Gezaulole Kigamboni ambapo mfanyabiashara aliyefahamika kwa jina la Hamis Said Luongo (38) alimuua mke wake aliyefahamika kwa jina la Naomi Marijani (36) kisha kuuweka mwili huo ndani ya shimo alilochimba katika banda la kufugia kuku lililopo nyumbani kwao na kuuchoma kwa kutumia magunia mawili ya mkaa na baada ya mwili huo kuteketea alichukua majivu akayaweka kwenye mfuko wa plastiki na kuondoka nayo kwa kutumia gari lake na kuyapeleka shambani kwake Mkoa wa Pwani kisha kuyazika na juu yake alipanda mgomba. Kabla ya kubainika, mtuhumiwa huyo alisambaza taarifa kuwa mke wake huyo ametoweka na hajulikani alipo kwa kipindi kirefu. Baada ya uchunguzi, chanzo cha tukio hilo kilibainika

kuwa ni wivu wa mapenzi. Mtuhumiwa alifikishwa Mahakamani na kuhukumiwa kunyongwa hadi kufa.

Serikali kupitia Jeshi la Polisi ina jukumu la kulinda maisha ya watu na mali zao na sio vinginevyo. Aidha, matukio yote yaliyoripotiwa yakihusisha watu mbalimbali kupotea, uchunguzi bado unaendelea hadi pale ukweli utakapopatikana wa nini kilichowatokea watanzania wenzetu.

Kwa upande wa matukio ambayo yalitokea na kuhusishwa na vitendo vya utekaji na wahusika wake bado hawajapatikana, Jeshi la Polisi linatoa wito kwa ndugu, jamaa na marafiki wa watu hao kuendelea kuwa watulivu wakati vyombo vya dola vikiendelea na uchunguzi wa matukio yanayowahusu ili kuweza kubaini uhalisia wa matukio hayo.

Ikumbukwe kuwa kitendo cha kusambaza taarifa za uongo ni kinyume cha sheria kwa mujibu wa kifungu cha 16 cha Sheria ya Makosa ya Mtandao namba 14 ya mwaka 2015 na adhabu yake ni kulipa faini ya kiasi cha fedha kisichopungua shilingi za kitanzania milioni tano (Tshs 5,000,000/=) au kifungo gerezani kisichopungua miaka 5 au vyote kwa pamoja, Hivyo ni vyema wananchi kutoa taarifa za kweli na zilizo sahihi ili zisaidie kupata ukweli wa tukio lililotokea kuliko kusambaza taarifa ambazo hauna uhakika nazo.

**Imetolewa na**:
Msemaji wa Jeshi la Polisi
Makao Makuu ya Polisi
Dodoma,Tanzania